

Changamoto za Mbinu za Kutathmini Tafsiri

*Maisha Laston Mwaipaja na Pendo Salu Malangwa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Ikisiri

Matokeo yoyote ya tafsiri ni vizuri yapimwe ufaafu wake kabla ya kupelekwa kwa watumiaji. Hii ni kwa ajili ya kujiridhisha kama kazi aliyoifanya mfasiri ina ubora unaotarajiwa kwa matumizi ya walengwa. Katika makala haya tumeangazia changamoto za matumizi ya mbinu nne za kutathmini tafsiri ambazo ni kufanya tafsiri rejeshi, kupima uelewekaji, kupima uasili na kupima ulinganifu. Mbinu hizi zimebainika kuwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ugumu wa utekelezekaji wa madai ya mbinu husika na kubana matumizi ya lugha. Msimamo wa makala haya ni kwamba, uamuzi wa mbinu ipi itumike kutathmini matini fulani ya tafsiri unapaswa kuongozwa na mbinu na nadharia iliyotumika kutafsiri matini husika. Hii ni kwa sababu mbinu na nadharia iliyotumika kutafsiri matini fulani ina athari kubwa katika matokeo, mwonekano na ujumbe wa matini lengwa. Aidha, katika makala haya inasisitizwa kwamba ni muhimu zaidi kwa yeyote anayetathmini matini ya tafsiri kutumia mbinu zaidi ya moja kutathmini matini moja ili kupata matokeo bora na yenye uhalisia. Vilevile, tumependekeza mbinu nyingine ya kutathmini tafsiri ambayo tumeiita mbinu ya uakifishaji.

Maneno Muhimu: Tafsiri, Changamoto, Tathmini, Mbinu na Nadharia

Utangulizi

Kutathmini ni kuangalia ubora na (au) udhaifu wa jambo au kitu fulani. Kwa mujibu wa BAKITA (2017) kutathmini ni kutafuta thamani ya kitu kwa kukadiria. Kwa mantiki hiyo, kutathmini tafsiri ni kuangalia ubora na (au) udhaifu wa matini za tafsiri kabla ya mchakato, wakati wa mchakato au baada ya kuhawilishwa kutoka kwenye matini chanzi (MC) kwenda kwenye matini lengwa (ML) (Malangwa, 2012). Kwa upande mwingine neno changamoto, Vide~Muwa (2016) wanaeleza kuwa ni tatizo analokabilia nalo mtu katika shughuli fulani. Wanaendelea kueleza kuwa ni kitu kinachomtia mtu katika hali ya kushindwa kuamua. Akifafanua zaidi kuhusu fasili ya changamoto, Msigwa (2016) anadai kuwa ni kazi au hali inayomjaribu mtu uwezo wake wa kutatua jambo. Hivyo basi, tunaweza kueleza kuwa changamoto ni hali kinzani ya kufanya jambo fulani. Kwa muktadha wa makala haya, wafasiri huwa wanakumbana na hali fulani ambayo inakuwa kinzani kwao kufanikisha zoezi la kutathmini tafsiri zao. Katika makala haya tutazitalii changamoto hizo kwa kila mbinu teule. Pia, tutatoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kufanikisha zoezi la kutathmini tafsiri licha ya changamoto anazokumbana nazo mfasiri anapotumia mbinu hizo katika zoezi husika. Kadhalika, mbinu za kutathmini tafsiri zipo nyingi lakini kwa muktadha wa makala haya tutaangazia mbinu nne tu ambazo ni kufanya tafsiri rejeshi, kupima uelewekaji, kupima uasili na kupima ulinganifu.

Tumeamua kushughulikia mbinu nne (Tafsiri rejeshi, kupima uelewekaji, kupima uasili na kupima ulinganifu) na kuacha mbinu mbili (kulinganisha matini na kupima usomekaji) zikiwa miongoni mwa mbinu sita za kutathmini tafsiri kutokana na sababu zifuatazo; Kwanza, mbinu ya kulinganisha matini ni mbinu muafaka ambayo haina changamoto katika utendaji wake kwa mtazamo wetu. Mbinu hii huhitajia mfasiri, mhakiki au mtu anayefanya tathmini ya tafsiri kulinganisha MC na ML ili kujiridhisha kama taarifa zote za MC zimeingizwa kwenye ML na kuona kama vipengele vyote vya kimuundo vimeshughulikiwa sawasawa (Taz. Malangwa, 2012). Mbinu hii inajaribu kutatua tatizo la udondoshaji wa taarifa muhimu za kwenye MC au uongezaji wa taarifa kwenye ML ambazo hazikuwapo kwenye MC. Kwa msingi huo, mbinu hii inafaa kutathmini tafsiri kwani haina changamoto katika utumizi wake kutokana na msingi wa kile inachokilenga kukibaini na kukiweka sawa katika ML kama kilivyokuwa katika MC.

Kwa upande mwingine, mbinu ya kupima usomekaji hatujaichambua changamoto zake kwenye makala haya kwani mbinu hii katika utendaji wake inaonekana kuwa sehemu ya mbinu ya kupima uasili. Mambo mengi yanayopendekezwa kufanyika kwenye mbinu hii yanafanana na yale yanayopendekezwa kufanyika kwenye mbinu ya kupima uasili. Mathalani, Larson (1984) anaeleza kuwa ni vyema wanaotathmini tafsiri kwa kuangalia uasili na usomekaji wakawa wahakiki waliobobea au wenye ujuzi wa kuandika katika LL. Vilevile, Malangwa (2012) akijadili kinachotakiwa kufanyika katika mbinu ya kupima uasili anaeleza yafuatayo:

Kwa kawaida, msomaji wa tafsiri husoma tafsiri huku akiwa na kalamu ya risasi mkononi mwake ili kupigia mistari au kuwekea alama sehemu ambazo hazisomeki vizuri au hazisomeki katika uasili. Baada ya kusoma yote, msomaji wa tafsiri hurejea tena kusoma kwenye sehemu alizozipigia mistari. (Malangwa, 2012:55).

Ukirejelea kwenye dondoo hapo juu, mwandishi alikuwa akielezea namna ya kutumia mbinu ya kupima uasili katika kutathmini tafsiri lakini wakati huo huo alikuwa akielezea masuala ya usomekaji ambayo ni sehemu ya mbinu ya kupima usomekaji. Kwa mantiki hiyo, tumeamua kuiacha mbinu ya kupima usomekaji badala yake tunavyoichambua mbinu ya kupima uasili na masuala ya usomekaji yanakuwa wameunganishwa humohumo.

Uteuzi wa baadhi ya mbinu (Tafsiri rejeshi, kupima uelewekaji, kupima uasili na kupima ulinganifu) na kuacha mbinu zingine (kulinganisha matini na kupima usomekaji) katika kuchambua changamoto zake umeukiliwa na uhakiki wa kina tulioufanya juu ya mbinu hizo zinavyofanya kazi na uhusiano wake katika kutathmini tafsiri. Uhakiki huo ndiyo uliotupa matokeo kuwa mbinu ya kulinganisha matini haina changamoto katika matumizi yake hivyo hatukuona haja ya kuichambua katika makala haya. Kwa upande mwingine, mbinu za kupima uasili na kupima usomekaji tulibaini kuwa zinafanana. Kutokana na sababu hizo ndipo tukaamua kuichambua mbinu mojawapo (kupima uasili) na kuiacha mbinu nyingine (kupima usomekaji). Sehemu itakayofuata baada ya kueleza mbinu iliyotumika kukusanya data na mkabala ulioongoza uandishi wa makala haya, tutafafanua misingi ya ufanyaji kazi wa kila mbinu teule, changamoto za kuzitumia kutathmini tafsiri na mapendekezo ya nini kifanyike kwa kila mbinu.

Mbinu ya Kukusanya Data na Mkabala

Mbinu iliyotumika kukusanya data za makala haya ni mbinu ya upitiaji wa machapisho mbalimbali. Machapisho yaliyopitiwa ni pamoja na vitabu, makala katika majarida matatu ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ambayo ni *Mulika, Kiswahili* na *Kioo cha Lugha*, pamoja na tasnifu na tazmili kutoka katika maktaba za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mbinu hii iliteuliwa kutokana na ukweli kwamba tafsiri inahusu matini zilizoandikwa. Kwa hiyo, vyanzo vya data vinavyotarajiwa kwa kiasi kikubwa ni machapisho. Aidha, baada ya data lengwa kukusanywa, mkabala wa kitaamuli ulitumika katika uandishi wa makala haya. Mkabala wa kitaamuli ni ule unaohusisha maelezo kwa kiasi kikubwa kuliko takwimu. Mkabala huu uliteuliwa kutokana na aina ya data iliyokusanywa, ambayo kwa kiasi kikubwa ni data ya kimaelezo pamoja na malengo ya makala haya, ambayo ni kufanya uchambuzi wa mbinu za kutathmini tafsiri na siyo takwimu.

Uchambuzi wa Mbinu za Kutathmini Tafsiri, Changamoto na Mapendekezo

Katika uchambuzi huu tutaanza na mbinu ya kufanya tafsiri rejeshi. Kwa kutumia mbinu hii, ML huhawilishwa na mfasiri mwingine (tofauti na mfasiri wa awali) kwa kuirejesha kwenye lugha ya MC. Mbinu hii hufanyika baada ya mchakato wa uhawilishaji kukamilika. Katika mchakato huu MC na ML zinabadilishana nafasi. Hii ina maana kwamba, matini iliyokuwa chanzi kwenye mchakato wa kawaida wa uhawilishaji inakuwa ML na kinyume chake kwenye tafsiri rejeshi. Katika mchakato wa kufanya tafsiri rejeshi, matini zinakuwa tatu badala ya mbili za awali, yaani matini ya lugha chanzi (MLC), matini ya lugha lengwa (MLL) na matini ya tafsiri rejeshi (MTR). Malangwa (2012) anashauri kuwa ili kupata matokeo bora na yenye uhalisia ya tafsiri rejeshi, mfasiri atakayefanya tafsiri rejeshi ni vizuri asiione iliyokuwa MC.

Kutokana na msisitizo wa mfasiri atakayefanya tafsiri rejeshi kutokusoma au kuoneshwa MC, ni vigumu sana kupata matini zinazowiana hasa kama mfasiri wa kwanza alitumia nadharia ya Skopos au mbinu ya kimawasiliano inayompa uhuru mkubwa mfasiri kuamua namna ya kufasiri ujumbe. Wakielezea uhuru alionao mfasiri anapotumia mbinu ya kimawasiliano kutafsiri, Mwansoko na wenzake (2015) wanadai kuwa mfasiri yuko huru kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali, utamaduni na mazingira ya lugha lengwa. Hii ina maana kwamba, mfasiri anao uhuru wa kuamua ni maneno gani mbadala ayatumie ili kufikisha ujumbe kwa jamii lengwa. Uhuru huo huleta matokeo tofauti zaidi endapo mfasiri atakuwa ametumia nadharia ya Skopos katika kufasiri MC kwenda ML. Pengine tudokeze kwa ufupi kuhusu nadharia ya Skopos. Mwasisi wa nadharia hii ni Mjerumani Hans. J. Vermeer miaka ya 1970. Msingi wa nadharia hii ni kwamba, matini hutafsiriwa kwa lengo fulani na kwa hiyo tafsiri lazima itimize lengo hilo. Akifanua zaidi kuhusu nadharia ya Skopos, Mpemba (2016) anadai kuwa matini moja inaweza kutafsiriwa kwa namna mbalimbali kutokana na kuwa na malengo tofautitofauti. Anaendelea kueleza kuwa, kwa mfano, tafsiri ya “*Mabepari wa venisi*” ilizingatia zaidi lengo la kuhubiri ujamaa, ingawa “*The merchant of Venice*” haikukusudiwa kufanya hivyo. Sasa katika mazingira ya uhuru wa namna hiyo kwa mfasiri, ni vigumu sana kutumia mbinu ya tafsiri rejeshi kupata matokeo yanayotarajiwa. Hebu tutazame mfano ufuatao:

Mfano wa 1.

MLC: Mr. Zapetero thanked **jubilant supporters** for a **clear victory** ...

MLL: Bwana Zapetero amewashukuru **wapiga kura wake** kwa kumpatia **ushindi huo...**

MTR: Mr. zapetero thanked **his voters** for providing him with **such a victory**...

Chanzo cha data: Fupi (2010:56-57) katika Malangwa (2012:62)

Kutokana na mfano wa kwanza (1) hapo juu, tunaona MTR ikiingiza taarifa mpya na kudondosha baadhi ya taarifa zilizokuwamo kwenye MLC. Kwa mfano, katika MTR kuna umilikishaji wa wapiga kura ambao haukuwapo kwenye MLC. Vilevile, ule ushindi wa moja kwa moja/wazi/mkubwa uliodokezwa kwenye MLC haujadokezwa kwenye MTR. Mfano mwingine ni tafsiri ya riwaya ya kiingereza ijulikanayo kama “*Things Fall Apart*” ambayo miongoni mwa tafsiri zinazotumika sana katika Kiswahili ni “*Shujaa Okonkwo*”. Endapo mtu ambaye hajawahi kuisoma au kuona riwaya hiyo akiambiwa afanye tafsiri rejeshi ya “*Shujaa Okonkwo*” atahawilisha kuwa ni “*Okonkwo The Hero*” matokeo ambayo ni tofauti kabisa na ilivyokuwa kwenye MLC. Hali hii inachagizwa zaidi na matumizi ya mbinu ya tafsiri ya kimawasiliano wakati wa uhawilishaji wa matini kutoka MLC kwenda MLL.

Mbinu hii ya kutathmini tafsiri (Tafsiri rejeshi) inapotumika hasa kwa matini ambayo ilihawilishwa kwa kutumia nadharia ya Skopos na mbinu ya kimawasiliano ni vigumu sana kupata matokeo halisi kama ilivyodokezwa kwenye mifano iliyodondolewa hapo juu. Hivyo basi, tunashauri mbinu hii itumike pale inapofanyiwa tathmini matini iliyohawilishwa kwa mbinu za neno kwa neno, tafsiri sisi na tafsiri ya kisemantiki ili kupata ulinganifu kati ya MLC na MTR. Vilevile, mbinu hizo za tafsiri ziambatane na nadharia za ulinganifu zinazohitajia kuwapo kwa ulinganifu wa kimuundo na kiathari kati ya MC na ML na si vinginevyo.

Mbinu ya pili ya kutathmini tafsiri ni kupima uelewekaji. Mbinu hii inahitajia kupima kama maudhui ya tafsiri yanaeleweka kwa wasomaji wa lugha lengwa (LL) au la. Malangwa (2012) anaeleza kuwa uelewekaji wa maudhui ya tafsiri unaweza kupimwa kwa tafsiri nzima endapo matini ni fupi au sehemu ndogo ya tafsiri kama matini ni ndefu. Anaendelea kueleza kuwa inashauriwa watu wanaoshiriki kupima uelewekaji wa maudhui ya matini wapewe tafsiri nzima au sehemu ndogo ya tafsiri ili waisome na kutoa majibu ya kile walichokielewa kutoka kwenye matini iliyotafsiriwa.

Changamoto kubwa ya kutumia mbinu hii kutathmini tafsiri ni pale inapoelekezwa kutumia sehemu ndogo ya matini ndefu kupima kueleweka kwake. Hii haiwezi kutupa matokeo yanayotarajiwa kwani matini inaweza kuwa na sura tofauti zenye ujumbe mkuu tofauti kwa kila sura. Vilevile, sura moja inaweza kuwa na ujumbe wa wazi unaoeleweka kwa wasomaji na sura nyingine

ikawa na ujumbe mgumu usioeleweka kwa uwazi. Hivyo basi, kuhitimisha kueleweka kwa matini kwa kutumia sehemu ndogo tu ya matini nzima ni kujidanganya wala haiwezi kukupa matokeo halisi ya tathmini ya tafsiri kulingana na kinachokusudiwa kupatikana baada ya zoezi kukamilika.

Kwa upande mwingine, kwa kawaida watu wana uwezo tofauti wa kuelewa mambo. Watu wawili wenye kiwango sawa cha kielimu wanaweza kuelewa jambo moja kwa namna tofauti. Sasa katika kupima uelewekaji wa matini, mtu anayetathmini tafsiri atatumia kigezo gani cha kuchukua maoni ya mtu mmoja aliyeelewa tofauti na kuacha maoni ya mtu mwingine aliyeelewa tofauti na yule wa kwanza?. Kwa muktadha huu inakuwa ni vigumu sana kutathmini matini kwa kupima kueleweka kwake kwa wasomaji wa LL.

Tofauti na tulivyoshauri kwenye mbinu ya tafsiri rejeshi kuwa inaweza kutumika kwa kuzingatia mbinu na nadharia iliyotumika kutafsiri matini kutoka MLC kwenda MLL, mbinu hii ya kupima uelewekaji haiwezi kuamriwa na mbinu wala nadharia iliyotumika kutafsiri MLC kwenda MLL na kutumika peke yake. Badala yake tunapendekeza kuwa, mbinu hii inaweza kutumika kwa kujaliza mbinu zingine lakini siyo kutumika peke yake kutathmini tafsiri.

Mbinu ya tatu ya kutathmini tafsiri ni kupima uasili. Mbinu hii ya kutathmini tafsiri inahitajia ML kusimama peke yake bila kuwa na harufu ya lugha ya MC. Msisitizo hapa ni kwamba zao la tafsiri (MLL) halipaswi kuwa na vionjo vyovyote vya MLC (Taz. Nida na Taber, 1982 na Malangwa, 2012). Vionjo vya MLC kwenye MLL vinavyodokezwa ni msamiati, istilahi, miundo na mtindo wa uwasilishaji. Mathalani, Malangwa (2012:55-56), anaeleza kuwa tafsiri inayotolewa inapaswa isomeke kana kwamba imeandikwa katika LL hiyo. Anaendelea kusisitiza kuwa tafsiri yoyote haipaswi kusomeka na kuonekana kwamba ni tafsiri kutoka lugha fulani. Kwa mantiki hiyo, mfasiri anatakiwa kuwa makini sana na kuwa mbunifu wa hali ya juu kuhakikisha zao la tafsiri yake lionekane liliandikwa katika LL na si kuonekana kama ni tafsiri kutoka lugha fulani.

Kiuhalisia kinachosisitizwa kupitia mbinu hii hakiwezekani katika muktadha wa tafsiri, hasa tafsiri za matini za kiutamaduni. Kutokuwezekana huko kunachagizwa na tofauti zilizopo baina ya lugha moja na nyingine. Tofauti hizo zipo katika mazingira, historia, isimu na utamaduni wa jamii moja na nyingine. Malangwa (2008 na 2012), Mshindo (2010), Baker (2011), na Mwansoko na wenzake (2015), wanadokeza kuwa tofauti za kijiografia, kihistoria, Kifalsafa, kifasihi, kiisimu na kiutamaduni baina ya lugha ambazo mfasiri anazifanyia kazi zinaweza kusababisha akose kisawe cha LC katika LL. Kwa upande wake Wanjala (2011), anaona kuwa lugha zinatofautiana sana kiutamaduni na hili ni tatizo kubwa sana kwa mfasiri hata kuliko tofauti za kiisimu. Katika kuweka msisitizo kuhusu tofauti za kiutamaduni, Mwansoko na wenzake (2015) wanaeleza yafuatayo; “Kwa hakika tofauti za kiutamaduni humpatia mfasiri matatizo (ya kifasiri) makubwa zaidi kuliko yale ya tofauti za kiisimu” (Mwansoko na wenzake, 2015:30). Katika mazingira ya namna hiyo, ni vigumu sana kuzingatia suala la uasili katika tafsiri za matini za kiutamaduni.

Malangwa (2014) alibainisha mambo ya kiutamaduni yanayoweza kuleta changamoto za tafsiri, ikiwa ni pamoja na maneno yanayohusu vyakula, vinywaji, mahusiano ya koo, shughuli za kiutamaduni, salamu na mifumo ya kisiasa. Kwa upande wake Jilala (2014), akieleza matatizo ya kiutamaduni kwenye tafsiri, alibainisha kuwa yapo katika viwango viwili ambavyo ni; tatizo la kutafsiri majina kutoka LC kwenda LL na tatizo la kutafsiri dhana za kiutamaduni kutoka LC kwenda LL. Mifano ifuatayo ni ushahidi mzuri wa jinsi ilivyochangamoto kutafsiri dhana na majina ya kiutamaduni kutoka utamaduni wa jamiilugha moja kwenda utamaduni wa jamiilugha nyingine kama inavyoonekana katika mfano wa 2 unaotolewa katika Jedwali la 1:

Jedwali la 1: Tafsiri ya Dhana na Majina ya Kiutamaduni

Na.	Kiswahili (MC)	Kiingereza (ML)
1.	Banda	Banda
2.	Kinyamkera	Kinyamkera
3.	Dungu	Dungu
4.	Mbege	Mbege

Chanzo cha Data: Jilala (2014:43)

Tukiabili mifano iliyotolewa na Jilala kwenye Jedwali la 1, tunabaini kuwa maneno yalivyokuwa kwenye MLC (Kiswahili) yametafsiriwa kwa kuhamishwa kama yalivyo kwenda kwenye MLL (Kiingereza). Tunadhani imetokea hivyo kwa mfasiri wa matini husika kutokana na kukosa visawe vya maneno hayo kwenye LL kulikosababishwa na tofauti za kiutamaduni baina ya lugha zinazohusika. Sasa ukitaka utathmini ubora wa tafsiri kwa kupima uasili, ni vigumu sana kupata matokeo halisi.

Jilala (2014) na Mwansoko na wenzake (2015) wametoa mapendekezo ya namna ya kushughulikia tafsiri ya maneno ambayo hayana visawe kwenye LL. Kwa mtazamo wao ni kwamba, maneno hayo yatafsiriwe kwa kuhamisha neno kama lilivyo na kulitolea ufafanuzi kulingana na jinsi linavyoeleweka katika utamaduni wa LC. Mifano iliyotolewa na wataalamu hao ni katika lugha za Kiswahili na Kiingereza zikiwa LC na LL kwa kubadilishana nafasi. Hebu tutazame mifano ya tafsiri iliyopendekezwa katika Majedwali hapa chini:

Jedwali la 2: Mapendekezo ya namna ya Kutafsiri Maneno ambayo hayana Visawe

Na.	Kiswahili (MC)	Kiingereza (ML)
1.	Kinyamkera	Kinyamkera (Kinyamkera is a small hut built at the back of the house for curing uncritical or normal diseases. It is also used for ritual purposes)
2.	Dungu	Dungu (A small traditional house used as a store to keep harvests which belong to a head of the family. The bottom of <i>dungu</i> is used as a pen for goats and chickens) is the kwere and Doe's house
3.	Banda	Banda (Banda is a type of house built with misalaka poles (thin but strong poles-it is believed that it can survive for more than 50 years)
4.	Mbege	Mbege (A Chaga's beer made up of millet or yellow banana)

Chanzo cha Data: Jilala (2014:43)

Tutazame pia data nyingine katika Jedwali la 3 hapa chini:

Jedwali la 3: Mapendekezo ya namna ya Kutafsiri Maneno ambayo hayana Visawe

Na.	Kiingereza (MC)	Kiswahili (ML)
1.	Ski	skii (mchezo wa kuskii)
2.	Skate	sketi (mchezo wa kusketi)
3.	Sunbathe	Jianika juani bila kuvaa nguo ili ngozi nyeupe (ya mzungu) iungulie na kuwa ya kihakawia

Chanzo cha Data: Mwansoko na wenzake (2015:31)

Kutokana na mapendekezo yaliyotolewa kwenye Majedwali hapo juu, tunadhani walichofanikiwa wataalamu hao ni kuisaidia hadhira lengwa kupata ujumbe lakini si uzingativu wa uasili wa tafsiri. Ukirejelea ufafanuzi wa *Dungu* na *Mbege* kwenye Jedwali la 2 hapo juu, utabaini kuwa mpaka maeneo vinakopatikana vitu hivyo kwenye jamii ya MLC yametajwa. Halikadhalika, ufafanuzi wa *sunbathe* kwenye Jedwali la 3 hapo juu, mpaka rangi ya mtu anayetakiwa kufanya hicho kitendo imetajwa. Sasa swali la kujiuliza; Je, hadhira ya MLL ambayo ni ya Kiingereza na Kiswahili mtawalia itakapokuwa inasoma matini hiyo itajua matini hiyo iliandikwa kwenye lugha yake na wala si tafsiri kutoka lugha fulani? Kwa ushahidi huu ni vigumu sana kupima uasili katika MLL.

Mapendekezo yetu kuhusu matumizi ya mbinu ya kupima uasili katika kutathmini tafsiri ni kwamba, siyo faafu zaidi kuitumia kutathmini tafsiri za matini za kiutamaduni kutokana na tofauti kubwa zilizopo baina ya lugha moja na nyingine kama ilivyobainishwa hapo juu. Kiuhalisia ni vigumu sana kupata tafsiri ambayo haina kabisa kabisa vionjo vyovyote vya LC kwenye MLL endapo matini inayofanyiwa tathmini ni ya kiutamaduni. Unaweza kuepuka vionjo vya kitahajia (Taz. Mifano kwenye Jedwali la 3 mfano wa 4) na miundo ya sentensi lakini ni vigumu sana kuepuka vionjo vya istilahi na msamiati hasa kama tafsiri imehusisha jamiilugha mbili tofauti. Kwa hiyo, tunadhani mbinu hii isitumike kabisa kutathmini tafsiri za matini za kiutamaduni.

Mbinu ya nne ni kupima Ulinganifu. Ulinganifu unaodokezwa kwenye mbinu hii ni ule wa kutumika kwa namna moja msamiati, istilahi au maneno yanayobeba maudhui ya MC. Kwa mfano,

ikiwa dhana fulani mfasiri ameitengenezea kisawe chake, anapaswa kutumia kisawe hicho kwa namna moja katika maeneo yote ambamo istilahi hiyo inajitokeza (Malangwa, 2012). Msisitizo hapa ni kwamba, istilahi fulani iliyotumika mwanzo kumaanisha kitu fulani, iwe hivyo hivyo kila itokeapo dhana ya namna hiyo kwenye matini nzima ya LL.

Ukiangalia kwa yakini madai ya mbinu hii ni kwamba, inajaribu kubana maana ya maana ilhali maana siyo tuli ni telezi, kwani inabadilika kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa kuzingatia nadharia ya maana kama matumizi, maana ya umbo la kiisimu ni matumizi yake katika muktadha lilipotumika. Kwa mantiki hiyo, mtu hapaswi kuuliza maana ya neno bali aangalie muktadha wa matumizi yake ili kung'amua maana (Taz. Ullmann, 1962; Lyons, 1987; Akmajian na wenzake, 2010 na Riemer, 2010). Vilevile, Dolet (1540) kama alivyonyukuliwa na Mpemba (2015) anatahadharisha kuwa mfasiri aepuke kutafsiri neno kwa neno kwani kufanya hivyo ni kuharibu maana ya MC na uzuri wa semo. Hivyo basi, kusisitiza ulinganifu wa istilahi katika ML ni kubana matumizi ya lugha kwa kulipa neno maana mahususi ilhali linaweza kuwa na maana nyingi tofautitofauti kulingana na muktadha wa matumizi.

Kwa mfano neno **“kata”** katika MLC ambayo ni Kiswahili likitafsiriwa katika MLL ambayo ni Kiingereza linaweza kuwa **“cut”**, au **“water container”** au **“ward”** kulingana na muktadha wa matumizi kwenye matini moja hiyo hiyo. Kwa kuzingatia madai ya mbinu ya kupima ulinganifu, mfasiri angeteua kisawe mahususi cha neno **“kata”** kuwa ni **“cut”** ingemuwia vigumu sana kuzingatia ulinganifu kutafsiri sentensi ya Kiswahili **“Raia wa kata ya Ipinda hushirikiana kwenye masuala yote ya kijamii”**. Angelazimika kutafsiri kuwa **“Citizens of Ipinda cut cooperates in all social issues”**. Tafsiri hiyo ingepotosha kabisa maana ya sentensi iliyorejelewa kwenye MC na pengine ingebua kitu kipya kabisa. Mfano mwingine ni tungo ya Kiswahili **“Anacheza mpira wa miguu”** katika Kiingereza itakuwa **“He/she is playing football”** lakini tungo **“anacheza muziki”** kwa ajili ya kuzingatia ulinganifu haiwezi kuwa **“He/she is playing music”** kwani kutakuwa na usisizi kwenye tafsiri husika, bali tafsiri faafu itakuwa **“He/She is dancing”** kulingana na muktadha wa matumizi.

Mbinu hii ikiambatana na mbinu zingine, inaweza kutumika kutathmini tafsiri kama na kama tu mfasiri ataitumia kwa tahadhari. Hii ina maana kwamba, ikiwa kisawe husika kimetumika kwenye muktadha A na B unaofanana basi ulinganifu uzingatiwe. Lakini kama muktadha A na B ambamo kisawe husika kimetumika ni tofauti, basi muktadha husika ndiyo uamue maana ya kisawe hicho na si kulazimisha suala la ulinganifu.

Mbinu nyingine ya Kutathmini Tafsiri inayopendekezwa

Tumependekeza kwenye makala haya kuwa mbinu ya kupima uasili isitumike kutathmini tafsiri za matini za kiutamaduni kutokana na ugumu wa kufikia madai yake ya MLL kutokuwa na vionjo vyovyote vya MLC kama tulivyofafanua hapo juu, lakini mbinu hii ikiambatanishwa na mbinu ya kupima usomekaji ina baadhi ya madai ambayo siyo ya uasili wa istilahi na msamiati wa MLL, ila yana umuhimu wa kuyafanya matokeo ya tafsiri za matini za kiutamaduni kuwa bora na ya kuvutia kwa wasomaji. Madai hayo ni pamoja na kuchunguza kama ML haisomeki vizuri, haina usahihi, haina mtiririko unaokubalika katika LL, na kadhalika. Ili kushughulikia masuala hayo tunapendekeza **mbinu ya uakifishaji** katika kutathmini tafsiri. BAKITA (2017:1065) linaeleza kuwa uakifishaji ni utumiaji wa alama za kiuandishi katika maandishi ili kumfanya msomaji azifuate na hivyo kuyafanya maandishi hayo yaeleweke vizuri kwa hadhira. linaendelea kueleza kuwa lengo ni kuleta usahihi wa kile kinachoandikwa. Kwa kuwa lengo la uakifishaji ni kuleta usahihi wa kinachoandikwa hivyo masuala kama makosa ya kitahajia, miundo isiyo sahihi na mengine yanayofanana na hayo yatashughulikiwa na mbinu hii. Mbinu hii tunapendekeza ifanyike mwishoni baada ya mbinu zingine kufanya sehemu zake. Itafanywa na mtu/watu maalumu wenye taaluma ya uhariri kwa lengo la kujiridhisha kama masuala ya uakifishaji yamezingatiwa kwenye MLL.

Hitimisho

Katika makala haya tumejadili na kutathimini mbinu nne zinazotumika kufanya tathmini ya tafsiri ambazo ni mbinu ya tafsiri rejeshi, mbinu ya kupima uelewekaji, mbinu ya kupima uasili na mbinu ya kupima ulinganifu. Katika mjadala huo tumeonesha namna mbinu hizo zinavyotumika na changamoto zake. Pia, tumetoa mapendekezo kwa kila mbinu ili kufanikisha kazi ya kutathmini tafsiri. Mtazamo wetu ni kwamba matumizi ya mbinu hizo katika kutathmini tafsiri yaamriwe na mbinu na nadharia iliyotumika wakati wa kutafsiri kutoka MLC kwenda MLL kwa upande wa mbinu ya tafsiri rejeshi. Kwa upande wa mbinu ya kupima uelewekaji tumeshauri isitumike peke yake bali ijalize mbinu zingine. Kuhusu mbinu ya kupima uasili tumeshauri mbinu hii isitumike kutathmini tafsiri za matini za kiutamaduni kutokana na utofauti mkubwa uliopo baina ya jamiilugha moja na nyingine kwenye masuala husika. Ilhali mbinu ya kupima ulinganifu tumeshauri itumike kwa tahadhari ikiwa ni pamoja na kutolazimisha ulinganifu pale kisawe kinapotumika kwenye muktadha tofautitofauti. Pia, tumependekeza mbinu nyingine ya kutathmini tafsiri ambayo ni mbinu ya Uakifishaji ili kushughulikia baadhi ya masuala yanayodokezwa na mbinu ya kupima uasili tuliyojipendekeza isitumike kutathmini tafsiri za matini za kiutamaduni lakini inadokeza baadhi ya mambo ya msingi yatakayofanikisha matokeo bora ya tafsiri za matini za kiutamaduni na zingine kwa ujumla. Kwa ujumla tunapendekeza kutumia mbinu zaidi ya moja kutathmini matini moja.

Marejeleo

- Akmajian, A., Demers, R.A., Farmer, A. K. na Harnish, R.M. (2010). *Linguistics: An Introduction to Language and Communication*, Toleo la 6. London: The Massachusetts Institute of Technology Press.
- Baker, M. (2011). *In Other Words: A coursebook on Translation*. Toleo la 2. London/Newyork: Routledge.
- BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Toleo la 2. Dar es salaam: Longhorn Publishers Limited.
- Jilala, H. (2014). “Matatizo ya Tafsiri katika Matini za Kitalii Nchini Tanzania”. *Kioo cha Lugha: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 12: 27 - 47
- Larson, M. L. (1984). *Meaning-based Translation: A Guide to Cross-language Equivalence*. New York: University Press of America.
- Lyons, J. (1987). *Semantics*. New York: Cambridge University Press.
- Malangwa, P. S. (2008). “Ukiushi katika Kufasiri Matini za Kifasihi: Mifano kutoka Tafsiri ya Julius Kambalage Nyerere: **Mabepari wa Venisi**”. *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 71: 24 – 33.
- Malangwa, P. S. (2012). “Mbinu Mbalimbali za Kutathmini Tafsiri”. *Kioo cha Lugha: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz.10: 50 – 69.
- Malangwa, P. S. (2014). “Challenges of Translating Cultural Expression in Teaching Kiswahili to Foreigners”. *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 77: 104 – 117.
- Mpemba, T. (2015). “Kufasiri, Kukalimani na Kurudufu Matini kwa Lugha Nyingine: Tulikotoka hadi Tulipo sasa”. *Kioo cha Lugha: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 13: 81 – 102.
- Mpemba, T. (2016). “Nadharia za Tafsiri na Ukalimani”. Katika H.Jilala (Mh.) *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilabi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Limited. Kur. 19 – 51.
- Mshindo, H. B. (2010). *Kufasiri na Tafsiri*. Zanzibar: Kiwanda cha Uchapaji Chuo Kikuu cha Chukwani.
- Msigwa, A. B. G. (2016). “Changamoto za Istilahi katika Uandishi wa Tasinifu za Uzamili wa Kiswahili Tanzania”. *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 79: 106 - 117.
- Mwansoko, H. J. M., Mekacha, R. D. K., Masoko, D. L. W. na Mtesigwa, P. C. K. (2015). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nida, E. na Taber, C. R. (1982). *The theory and Practice of Translation*. Shanghai: Foreign Language Education Press.
- Riemer, N. (2010). *Introducing Semantics*. New York: Cambridge University Press.
- Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. (2020). *Istilabi za Utafiti na Maneno Husiani*. Dar es Salaam: TUKI.

- Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. (2021). *Mwongozo wa Uandishi wa Tasnifu/Tazimili na Kazi mbalimbali za Kitaaluma*. Dar es Salaam: TUKI.
- Ullmann, S. (1962). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.
- Vide~Muwa. (2016). *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.
- Wanjala, F. S. (2011). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kwa Shule, Vjuzo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Education Publishers (I) LTD.